Usimamizi wa Utalii Unaozingatia Hali ya Mazingira Kijamii

TAARIFA YA UCHUNGUZI WA AWALI

Oktoba 2009

Utalii kwa Vizazi Vijavyo

HONEYGUIDE FOUNDATION
Ujamaa Community Resource Trust
TASConsult
Ecosystems Grants Programme EGP THE NETHERLANDS
SAND COUNTY FOUNDATION
Jumuiko la Maliasili Tanzania
Tanzania Natural Resource Forum

YALIYOMO

1. Kuutambulisha mradi 2
2. Muhtasari mkuu 3
3. Historia 4
4. Njia ya kufanya kazi 4
5. Matokeo 5
   5.1 Usimamizi wa matumizi ya ardhi ya vijiji 5
   5.2 Usimamizi na uhifadhi wa maliasili 6
   5.3 Upanuzi wa ajira na riziki 7
   5.4 Utawala na uwajibikaji 8
   5.5 Usimamizi na maendeleo ya utalii 10
6. Hitimisho na mapendekezo 11
7. Kuhusu washiriki… 12

1. KUUTAMBULISHA MRADI

Lengo la mradi huu ni kutengeneza mbinu mpya wa namna ya kuwashirikisha jamii katika kupanga utalii, ili jamii na wawekezaji wa biashara ya utalii wanaweza kuiga na kufaidika. Mradi huu unaratibiwa na Jumuiko la Maliasili Tanzania na kutekelezwa na timu ya wawakalishi wa JMT, Ujamma Community Resource Trust (UCRT), Honegyuide Foundation na TasConsult, na inafadhiliwa na IUCN (Ecosystem Grants Programme) na Sand County Foundation (Bradley Fund for the Environment). Eneo la mradi kijiografia ni Wilaya ya Ngorongoro katika vijiji vya Piyaya, Engaresero, Pinyinyi na Arash na inatekelezwa muda wa Aprili 2009 hadi Machi 2010.

Madhumuni ya mradi

1. Kutengeneza mipango shirikishi ya kuratibu shughuli za utalii katika vijiji vinne
2. Kutengeneza mwongozo kutokana na warsha, uzoefu na shughuli mbalimbali za mradi ambazo zitaweza kutumika na wawekezaji – wanajamii katika shughuli zao za utalii

Kuutambulisha uchunguzi wa awali

Uchunguzi wa awali uliofanyika mwezi Mei na Juni 2009 uliundwa kusaidia mahitaji mbalimbali. Maswali yalitokana na viashiria vya mradi na umekusudia kupata taarifa ambazo zitatumika kama msingi wakati wa tathmini mwishoni mwa mradi na baadae. Kwa kuongezea uchunguzi ulikusudia kuteka habari ambazo zitawawezesha timu ya mradi kufahamu mahitaji na matakwa ya wadau mbalimbali na kutoa habari zitakazoongoza mradi kutimiza malengo. Pia habari zinatoa taarifa za muhimu kwenye warsha na zinaweza kuwa za manufaa kwa wadau mbalimbali.

Picha zote ni za Gian Schachenman (kasoro ukurasa wa mwisho)

*Ramsar ni mji katika nchi ya Iran. Mkataba wa Ramsar ni wa kuhifadhi ardhi oevu zenye umuhimu wa kimataifa hasa kwa ajili ya makazi ya ndege-maji, na ni wa kimataifa ili kuhifadhi na kutumia ardhi oevu kwa njia endelevu.

2. MUHTASARI MKUU

Eneo la uchunguzi wa awali wa mradi ni vijiji vinne vya Pinyinyi, Engaresero, Arash and Piyaya. Katika vijiji hivi vyote kutoa kijiji cha Pinyinyi kuna biashara ya utalii ambayo inafanyika kwa miaka mingi na kila mojawapo ya hizi kampuni ina uzoefu wa biashara ya utalii na pia wanafanya kazi zao katika maeneo mengine katika Tanzania.

Uchunguzi wa kaya ulithibitisha kuwa jamii ya mahali hapa wanatambua vizuri maliasili zilizopo katika vijiji vyao. Hata hivyo, uhifadhi wa maliasili hizi ndani ya kijiji sio wa kuridhisha na hauwashirikishi vya kutosha wanakijiji. Ni dhahiri hakuna ushiriki wa wadau mbalimbali katika uhifadhi wa maliasili. Kwa mfano, Ziwa Natron ni eneo kubwa lenye maji mengi kuliko yote yaliyoko ndani ya eneo la mradi. Ziwa linapendekezwa kuwa eneo la Ramsar*, lakini hakuna kiashiria kinachoonyesha kwamba serikali ya kijiji na wanakijiji wana ufahamu wa haya maendeleo wala yana maana gani kwao.

Wanyamapori wanasimamiwa na Idara ya Wanyamapori. Hata hivyo, kutokana na uungwaji mkono mdogo kutoka Idara ya Wanyamapori au mamlaka za wilaya, mamlaka za viijiji wameanzisha usimamizi wa migogoro kati ya wanyamapori na binadamu. Moja ya mfano wa ushirikiano kati kijiji na kampuni za utalii uliopo kwa pamoja wameanzisha mpango wa uhifadhi ambao unahusisha kuchangia mfuko wa fedha wa kuwalipa fidia wananakijiji waliopoteza mifugo yao kutokana na kuliwa na wanyamapori.

Vijiji vya Piyaya, Arash na Engaresero vyote vina kamati ambazo zina majukumu katika shughuli za mazingira na utalii. Utafiti wa awali umepima utambuzi wa vyombo hivi na wajibu wake. Imegundulika kuwa katika vijiji vyote kuwa muundo wenye kutawala maliasili na utalii, ikihusisha wajibu na majukumu yake, haufahamiki miongoni mwa wananchi kwa ujumla. Serikali za vijiji vyote wameomba mafunzo na msaada kuendeleza utawala na usimamizi wa utalii. Hata hivyo, uongozi wa kijiji na wanakijiji wa ufahamu wa maliasili na vivutio muhimu vya utalii vilivyomo katika vijiji vyao, wana ukosefu wa elimu ya utalii kama biashara na nafasi ya kutambua bidhaa mahususi ambazo zitatoa msingi thabiti kwa kudalali sehemu mipango au mikataba yenye manafaa na mikakati inayohusika na usimamizi maendeleo ya utalii.

Muundo wa ada kwa bidhaa za utalii unatofautiana kutoka kijiji hadi kijiji. Haiko dhahiri jinsi upangaji wa ada ilivyofikiwa. Imefahamika kuwa ada inayotozwa na tawala nyingine kama Idara ya wanyamapori na ada za viingilio kwenye mageti mbalimbali zinazotozwa na mamlaka za wilaya, zinatishia ushindani wa bidhaa za utalii.

Utafiti katika kaya umeonyesha kuna maombi yanayojirudia kwa wanachama kutoka vijiji vyote kuhusu uwazi katika mikataba, mapato, na michango itolewayo kwa kijiji.

Wanakijiji wanahisi ukosefu wa taarifa kuhusu mikataba ya shughuli za utalii, inayowaathiri uwezo wao kuhoji uongozi wa kijiji. Kwa mfano kijiji kimoja kimeonyesha kulikuwa hakuna mikataba ya shughuli zozote za utalii. Hatahivyo, mkataba wa sasa uliandaliwa na mwekezaji. Hivyo, kuna ufahamu mdogo juu ya ubunifu wa uhisani mbalimbali uliopo kijijini pamoja na jumla ya mapato ya michango iliyowekezwa kwenye maendeleo ya kijiji kupitia utalii.

Kampuni za utaliii na serikali za vijiji hawakuwa na uelewa sawa wa wajibu na maudhui ya mikataba waliyoingia; hii inazidi kujionyesha zaidi kwa kuwepo kwa uvunjaji mbalimbali wa ahadi za mikataba kwa pande zote mbili. Imeonekana wazi kuna utofauti wa mawasiliano rasmi yaliyopo kati ya wawekezaji na serikali ya kijiji. Wengi wameegemea kwenye mawasiliano yenye kusudi muhimu na ni kijiji kimoja kina mikutano ya kawaida. Nafasi na Majukumu ya pande zote mbili pia hayako wazi na haukuwa wazi ukihusisha ufahamu wa mwongozo na kanuni zilizopo kwa watekelezaji wa utalii. Vyovyote vile hakuna mwongozo uliokuwepo kwa baadhi ya vijiji au mwongozo uliopo ni tofauti kati ya wawekezaji na serikali ya kijiji. Pia kulikuwa hakuna utaratibu wa kutathmini utendaji wa hiyo miongozo au sheria ndogondogo.

Mchango wa ujasiriamali wa kiutalii katika upanuzi wa ajira na kipato cha maisha unazuiwa na sababu kuu mbili: kwanza jamii inaishi katika maeneo ambayo ni kame na wametegwa kijiografia toka kwenye shughuli za utalii hivyo kukosa soko na hali sio nzuri, na pili ni kwamba wengi wa watu wa mahali hapa wana elimu ndogo na kwahiyo wanaweza kumudu baadhi ya nafasi zenye mahitaji machache ndani ya shughuli za utalii. Upungufu wa mazingira ya ajira na juhudi chache za kuendeleza sekta hii zina athari kubwa katika mawazo ya jamii ya mahali hapa na kwa upande wa utalii moja kwa moja kustawisha uchumi wa kaya.

3. HISTORIA

Vijiji vyote vinne vilivyo katika uchunguzi wa awali vyote viko ndani ya wilaya ya Ngorongoro, kijiji cha Arash na kijiji cha Piyaya ni majirani na vina bidhaa za utalii za kufanana, kijiji cha Engaresero na kijiji cha Pinyinyi ni majirani,hata hivyo ni kijijij cha Engaresero ndicho kina bidhaa thabiti za utalii. Kijiji cha Pinyinyi wana miradi kiasi toka kwa wawekezaji. Idadi ya watu katika vijiji vyote vitatu ni kati ya watu 4,500 hadi watu 4,800, kijiji cha Pinyinyi kina idadi kubwa ya watu 6,392.

Vijiji vyote vina msaada kutoka taasisi zisizo za kiserikali mbalimbali, hii imelenga zaidi kwenye maendeleo ya kijiji kwa kujengewa uwezo kupitia mashirika ya OXFAM, Ereto, na UCRT. Ni Piyaya na Arash tu waliopata msaada kama vile ufadhili wa shule, kupewa paneli za umeme wa jua, toka kwa wawekezaji wa utalii ambao wana mkataba nao. Kwa ujumla shughuli za utalii ndani ya vijiji vyote zinafanya na kutoa uzoefu wa ukambikaji, matembezi, shughuli za asili, safari za upigaji picha na safari za uwindaji.

4. NJIA YA KUFANYA KAZI

Dodoso liliandaliwa kwa kuzingatia viashiria vya mradi, na zilibadilishwa kwa makundi matatu tofauti ya wasailiwai: daraja la kaya, daraja la serikali ya kijiji na wawekezaji wa utalii. Uchunguzi ulifanywa na timu ndogo toka UCRT na Honeyguide Foundation katika eneo la mradi katika vijiji vya Piyaya, Arash, Pinyinyi na Engaresero.

Usaili wa serikali ya kijiji: Wanatimu walifanya mahojiano na viongozi wawili wa viijiji katika kila kijiji, ambapo ilifanyika kwa siku moja kwa kila sehemu. Pia walikusanya nyaraka muhimu na kumbukumbu toka kwa viongozi kuthibitisha taarifa zilizokusanywa.

Uchunguzi katika usawa wa kaya: Kusudi la kufanya uchunguzi wa kaya ilikuwa ni kukusanya taarifa na kupata mtazamo wa jamii kwa ujumla kuhusu shughuli za utalii ndani ya kijiji chao. Wanachama toka kaya 20 walihojiwa katika kila eneo ndani ya kijiji, kwa lengo la kupata kundi wakilishi la jamiii ya mahali hapa. Wahojaji walitumia mwongozo wa wasailiwa wanne toka kila makundi yanayofuata:

- Ambao wameajiriwa na kampuni za utalii (mlinzi, mkuu wa msafara, mpishi)
- Ambao hawajaajiriwa lakini wanafaidika na utalii (kama kuongoza matembezi huru au kutengeneza shanga, mwenye duka n.k)
- Ambao hawajihusishi na utalii; wanaishi mbali au hawaoni watalii
- Ambao wanaishi karibu na eneo la utalii lakini hawafaidiki mojakwamoja, maboma yao yapo karibu na kambi au barabara lakini hawauzi vitu au kuajiriwa na shughuli za utalii
- Wahojiwa kidharura toka kwenye jamii

Zaidi, wasailiwa katika mahojiano sharti watoke katika maboma au maeneo tofauti, wenye umri tofauti, na mchanganyiko wa wanaume na wanawake ili kuhakikisha unapata mtazamo anuai.

Uchunguzi wa waendesha utalii: Dodoso zilisambazwa kwa mawakala wa utalii tisa kwa njia ya barua pepe na sita walijibu. Mawakala wa utalii waliochaguliwa wote ni wawekezaji katika vijiji vya mradi. Waendeshaji wote wa Arash na Pinyinyi walijibu, wachangiaji wakuu wa Piyaya walijibu na Engaresero mmja alijibu.

5. MATOKEO

Dodoso kamilifu zimefupishwa katika muundo wa jedwali kwa kila kundi la msailiwa, na matokeo yalilinganishwa na kutathminiwa ili kupata hitimisho kuhusu shughuli za utalii katika eneo husika. Ifahamike kuwa taarifa zote zilipatikana toka wajibu wasailiwa mbalimbali na inaakisi maarifa yao, uelewa na mtazamo wa hali. Kama taarifa haziko sahihi, watunzi wa taarifa hii anaomba radhi ila anasisitiza kuwa hizi taarifa zimerekodiwa kwa nia njema.

Dodoso zinapatikana ukiandika barua pepe kwa info@tnrf.org.

5.1 USIMAMIZI WA MATUMIZI YA ARDHI YA KIJIJI

Ardhi iliyotengwa kwajili ya utalii: Vipimo vya eneo la kijiji ni vya kukadiria na vinatofautiana toka kijiji kimoja hadi kingine. Kijiji cha Engaresero kina eneo dogo kuliko vijiji vyote ambalo ni kilometa za mraba 1,045 kikifuatiwa na Arash chenye eneo la kilometa za mraba 1,950 na Piyaya chenye kilometa za mraba 2,700. Eneo kubwa la Piyaya lipo ndani ya Mamlaka ya Uhifadhi wa Eneo la Ngorongoro (NCAA). Rekodi ya eneo la kijiji cha Pinyinyi haikupatikana.

Katika uchunguzi wa awali vijiji vitatu waliambiwa wakadirie eneo la ardhi lililotengwa au kutumiwa kwa ajili ya utalii na walitaja ni kati ya asilimia 20 hadi 35 ya arhi yao, hii kwa haraka inakadiriwa kuwa Piyaya ina eneo kubwa la mraba kilometa za mraba 810 kwa ajili ya utalii, ila taarifa hizi zitakuwa za kupotosha endapo eneo limehusisha NCAA na hivyo hakuna mapato yatakayopatikana kwajili ya kijiji, Arash kinafuta kikiwa na eneo la kilometa za mraba 682 na Engaresero likiwa na eneo dogo la kilometa za mraba 209 lililotengwa kwa ajili ya utalii.

Mpango wa Matumizi ya Ardhi: Kati ya vijiji vinne, ni kijiji cha Engaresero chenye mpango na cheti cha umiliki. Arash wana mpango wa matumizi ya ardhi ila bado hawajasajili kutokana na mgogoro wa mipaka ya Malambo. Majadiliano yanaendelea baina ya serikali mbili za kijiji. Piyaya wana rasimu ya mpango ila wanatakiwa kutatua mgogoro wa mpaka wa kijiji na Malambo, majadiliano yako hatua za mwisho baina ya pande zote mbili chini ya uongozi wa serikali ya kijiji na baraza la wazee. Pinyinyi hawana mpango wowote wa matumizi ya ardhi na wana mgogoro wa mpaka na Oldonyo Sambu.

Utawala wa ardhi: Shughuli za kijiji na ardhi zinadhibitiwa na serikali ya kijiji. Hata hivyo kuna mawakala au bodi ya usimamizi ambayo pia inadhibiti rasilimali zilizo katika ardhi ya kijiji. Kimsingi NCAA na idara ya wanyamapori wana mamlaka juu ya ardhi, maliasili na wanyamapori kwa pamoja. Hata hivyo, uhusiano baina ya hizi mamlaka na kijiji inaonekana ni mbaya hasa idara ya wanyamapori hakuna taarifa zinazo onyesha wao kutembelea au kukutana na wanakijiji. TANAPA inapakana na Kijiji cha Arash na inakipatia msaada kijiji lakini haikutani na mamlaka za kijiji. Kutokana na uchunguzi uliofanyika, idara ya wanyamapori na NCAA hawajatoa mchango wowote katika maendeleo ya kijiji. Hii imeleta mgogoro juu ya nani anamiliki ardhi na haki ya kuitumia, hasa kwa kufuata maelezo ya sheria ya Wanyamapori.

Uongozi wa kijiji wanafahamu vizuri chanzo cha mgogoro kati ya uwindaji na utalii na "kinyang'any'iro cha rasilimali" kitisho kinawagusa na wanafahamu hitaji la kutatua hili jambo. Hata hivyo wana mikakati michache kwa sasa.

Migogoro juu ya ardhi na rasilimali: Migogoro michache kuhusu matumizi na usimamizi wa ardhi katika kijiji ilinukuliwa. Kijiji cha Pinyinyi kimeonyesha mgogoro baina ya uongozi wa kijiji na jamii juu ya eneo lililo chanzo cha maji. Engaresero wana mgogoro wa kufanana wa kukata miti katika ardhi ya kijiji. Kijiji cha Arash kimeonyesha hakuna mgogoro kwa sababu ya kuwepo mpango wa matumizi ya ardhi ingawa kwa kiutaratibu bado hujasajiliwa. Vijiji vyote wamesema hawana migogoro ya matumizi ya ardhi na shughuli za utalii.

5.2 USIMAMIZI NA UHIFADHI WA MALIASILI

Maliasili katika vijiji zinasimamiwa kwa kiasi kikubwa na serikali ya kijiji, ila vyombo vingine vya usimamizi toka nje ya kijiji wana majukumu maalum kama idara ya wanyamapori inaangalia wanyamapori, maeneo ya Ramsar, Ziwa Natron na Ardhi oevu. Uchunguzi wa awali umepeleleza mtazamo na uelewa wa serikali ya kijjiji na wanakijiji kuhusu usimamizi wa maliasili katika ardhi ya kijiji, ukizingatia kwa misingi ya kuwa ardhi hii ni sehemu muhimu ya vivutio vya utalii ndani ya kijiji.

Sheria ndogondodo za kijiji za kusimamia maliasili: Kwa ujumla, vijiji vitatu, Engaresero, Arash na Piyaya wa sheria ndogondogo za kusimamia maliasili. Hata hivyo, sheria zote zinasubiri kuidhinishwa na wilaya kabla haijaanza kutumika kijijini. Pinyinyi hawana sheria ndogondogo yoyote. Hakuna nakala yoyote ya sheria ndogondogo ilikuwepo wakati wa uchunguzi wa awali, hivyo maudhui ya hizi sheria ndogondogo hayakuangaliwa kwa umakini.

Ushirikishwaji na hamasa ya jamii: Uchunguzi wa kaya imethibitisha wananchi wanatambua vizuri maliasili zilizopo katika kijiji, na uongozi wa kijiji wanawahabarisha wanachama kupitia mkutano mkuu wa mwaka (MMM) na mikutano mingine inayohusu masuala mbalimbali ya uhifadhi yenye kuathiri kijiji. Kwa ujumla uongozi wa kijiji na wanachama hawako makini katika uhifadhi wa maliasili na hawahusishi wanakijiji ipasavyo. Shughuli maalum zinabadilika toka kijiji kimoja hadi kingine inategemea na mazingira ya pekee ya utalii katika kila kijiji, na msaada wa serikali kujulisha na kuunga mkono kutoka wanakijiji. Hakuna taarifa yeyote ya jitihada ya uhifadhi katika kijiji cha Arash, na ukifikiria uchunguzi wa kaya ambapo asilimia 80 ya wahojiwa hawakuwa wanatambua kampeni yeyote ya uhifadhi na salimia 20 ya wahojiwa wanatambua vizuri kuwa hakuna jitihada yoyote.

Maji na ardhi oevu: Ziwa Natron ni eneo kubwa kuliko yote lenye maji katika eneo la mradi, na limependekezwa kama eneo la Ramsar. Hata hivyo idara ya wanyamapori haijawatembelea na kujulisha kijiji kuhusu mlolongo wa mambo ya RAMSAR, hakuna kiashiria kwamba serikali ya kijiji au wanachama wanafahamu juu ya maendeleo na yana faida gani kwao. Kikamilifu mlolongo wa mambo ya Ramsar lazima kushughulikiwa ili kuzuia migogoro na kutokuelewana kuhusu mapendekezo ya kubadili hadhi ya ziwa. Uchunguzi wa awali umeandika kwamba wakazi wa Pinyinyi kiasi kidogo wana migogoro kwenye usimamizi maeneo fulani yaliyo vyanzo vya maji na wanaendelea kuwaadhibu wale wote wanaokiuka amri ya baraza la kijiji kuhusu kuhifadhi wa eneo. Zaidi ya yote asilimia 55 ya wakazi wa kijiji cha Pinyinyi walihudhuria mkutano kujadili maeneo yaliyo na vyanzo vya maji. Hata hivyo migogoro inaendelea tokea.

Misitu: Hakuna migogoro ya msitu iliyonukuliwa katika uchunguzi wa awali isipokuwa Engaresero ambapo uongozi wa kijiji unatumia sheria ndogondogo kulinda msitu wenye migunga katika kijiji. Jumla ya asilimia 70 ya kaya za Engaresero walihudhuria mkutano kujadili suala hili.

Wanyamapori: Wanyamapori Tanzania wanasimamiwa na Idara ya Wanyamapori. Hata hivyo mamlaka za kijiji wamechukua hatua ya kisimamia migogoro baina ya wanyamapori na binadamu kwa sababu ya msaada mdogo kutoka mamlaka ya Idara ya wanyamapori au wilaya.

Katika kijiji cha Piyaya na Arash Morani wa kimasai huwinda simba mojawapo ni kuonyesha ujasiri/ushujaa au kulipiza kisasi pale mifugo yao inapouawa na simba, kijiji cha Arash walifanya mkutano kuongeza utambuzi wa kuhifadhi simba, hata hivyo, uchunguzi wa kaya umeonyesha ni asilimia 40 tu ya wakazi wa kijiji walihudhuria. Uwindaji wa simba imeonekana ni tatizo linaloendelea kwa kampuni za utalii ambazo uwepo wa simba kama sehemu ya bidhaa zao una thamani kubwa mno. Katika kijiji cha Arash tembo wanaharibu mazao na mara chache huua watu. Ingwa kijiji wametaarifu suala hili kwa Idara ya wanyamapori na halmashauri ya wilaya, mwitikio uliopo ni mdogo. Mbogo wanaonekana kama ni tishio kwa ng'ombe hasa Kijiji cha Piyaya na Arash

wana hamisha magonjwa kwenda kwa ng'ombe na wanashindana katika malisho na maji. Hata hivyo kijiji wanafikiri hakuna wanalowezakufanya kuhusu tishio hili. Katika kijiji cha Engaresero, nyani wanahusika katika uwindaji wa watoto wa mbuzi. Mara nyingine mgogoro umetaarifawa kwa mamlaka za wilaya bila jibu lolote.

Katika kijiji cha Piyaya, utazamaji wa Mbwa mwitu hivi karibuni umekuwa wa mara kwa mara na wameongeza moja ya kivutio muhimu cha watalii. Hata hivyo mbwa mwitu wamekuwa wakiwinda mifugo mara kwa mara na hivyo kuhatarisha uwepo wao kwa kuchochea kulipiza kisasi toka wafugaji wa kimaasai. Kijiji kwa ubia na kampuni za utalii wameanzisha mfuko wa fidia, ambapo pande zote huchangia mfuko kulipa fidia kwa wanakijiji waliopoteza mifugo yao kwa mbwa mwitu. Ari hii imethibitisha mafanikio kwa kuwa mbwa mwitu wote wameendelea kuwepo katika eneo kwa ujumla muda wote. Hata hivyo taarifa ya ni kiasi gani wamechangia haiko wazi. Katika uchunguzi wa kaya asilimia 55 ya wasailiwa wanaufahamu wa mfuko na wamehudhuria mikutano kuzungumzia jitihada za uhifadhi.

Mbuga za nyasi: Katika mpango wa matumizi ya ardhi kwa Arash na Engaresero, maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya malisho yamebainishwa dhahiri. Piyaya na Pinyinyi hawana mpango wa matumizi ya ardhi, isipokuwa wanatumia mapatano ya kimila ya kugawa ardhi na malisho.

5.3 UPANUZI WA AJIRA NA RIZIKI

Kumekuwepo na umakini hafifu katika suala la upanuzi wa maslahi na ajira kwa jamii mahalia ndani ya eneo la kazi la kampuni. Katika vijiji vyote vinne ni watumishi wachache wanatoka katika jamii ya mahalia na mahitaji machache yananunuliwa eneo mahalia. Ajira kwa wenyeji ni ya msimu, ya muda maalum na ni kwa wanaume. Utafiti umepata mfano mmoja tu wa mwajiriwa mwanamke. Hakuna nafasi za mafunzo kwa wazawa zilizopo zaidi ya mafunzo ukiwa kazini.

Wengi wa wafanyabiashara ndogondogo ambao wanajihusisha na kampuni za utalii ni ama wana maduka yanayouza vitu vinavyo hitajika mara chache au biashara ndogondogo ya vitu vya utamaduni kwa wanawake wanaojitegemea. Wajasiriamali wadogo na wa kati hawatoki nje ya maeneo haya mawili na kungia kwenye bidhaa kama vile nyama, maziwa, mboga, kuku au uzalishaji wa mayai.

- Katika **kijiji cha Arash** kampuni za utalii zimeajiri hadi wanakijiji 27 kwa msingi wa muda maalum, na wote ni wanaume. Mafunzo yametolewa kwa njia ya kawaida. Pia kijiji cha Arash wana juhudi binafsi ambapo kampuni ya utalii huchangia dola za kimarekani 4 (US$ 4) kwa kila mteja kwenye mfuko wa wanawake.
- Katika **kijiji cha Piyaya** kampuni za utalii zimeajiri watumishi wa kudumu jumla ya wazawa 22. Nyongeza ya jumla ya watu 15 huajiriwa kwa msingi wa msimu (Desemba hadi Aprili). Kijiji kina boma la utamaduni ambapo kuendelea kutembelewa kwa boma na watalii huenda kutawasaidia wanawake maskini na na kuwapa nafasi ya kuuza kazi za shanga. Wakati mwingine waendeshaji utalii hununua kutoka kwenye maduka yaliyopo.
- **Kijiji cha Engaresero** kina mtiririko mzuri wa biashara kupitia ununuzi wa vitu katika maduka yaliyopo kijijini, yanayofikia zaidi ya shilingi milioni 10 za kitanzania kati ya mwaka 2006 na 2009. Pia wanawake wa Engaresero wana mradi wa kazi za ushanga ambao unasimamiwa na serikali ya kijiji. Mmoja wa waendeshaji utalii ameajiri watu saba kwa msingi wa muda wote, na watu 2 kwa msingi wa muda maalumu, wamepewa mafuzunzo ya kazi, na pia yameangalia maendeleo ya uongozi. Wakati wa kukusanya uchambuzi wa awali, mmoja wa waendeshaji utalii mkubwa katika eneo hakujibu, hivyo hatuna taarifa zilizo kamilika.
- Kwa bahati mbaya **kijiji cha Pinyinyi** hakina watalii na hivyo hakuna faida za kiuchumi zinazo weza kuandikwa.

5.4 UTAWALA NA UWAJIBIKAJI

Uchunguzi wa awali pia umepeleleza uwajibikaji na jitihada za serikali ya kijiji kuanzisha muundo katika kijiji kusimamia utalii na maliasili.

Ufahamu wa jamii kuhusu muundo wa utawala

Vijiji vya Piyaya, Arash na Engaresero wana kamati inayohusika na shughuli za mazingira na utalii. Uchunguzi wa awali umetathmini kaya juu ya ufahamu wa hizi kamati kwa kudadisi mhojiwa kama anatambua uwepo wa kamati, dhima yake na wanachama. Ufahamu wa kaya ni tofauti toka kijiji hadi kijiji. Ni dhahiri katika vijiji vyote kwamba wananchi kwa ujumla hawafahamu muundo wa utawala, dhima na wajibu wa usimamizi wa maliasili na utalii. Serikali za vijiji vyote wameomba msaada wa kuendeleza utawala, hasa kupitia mafunzo na msaada katika maeneo yafuatayo:

- Udhibiti wa fedha na utaratibu
- Usimamizi wa mazingira
- Msaada wa sheria zaidi kuhusu mapatano ya mikataba na uendelezaji

Ufahamu wa jamii kuhusu utawala wa utalii katika ardhi ya kijiji

Kila Serikali ya kijiji imeonyesha kuwa mkutano mkuu wa kijiji ndio njia pekee ya kupasha habari wanakijiji kuhusu mapato yaliyopatikana kutokana na utalii na hakuna utaratibu mwingine wa kupasha habari uliopo. Sio la kushangaza, uchunguzi wa kaya umeonyesha ufahamu mdogo kutoka kwa wanakijiji kuhusu mapoto kutokana na utalii. Uwazi wa mikataba baina ya kijiji na waendesha utalii pia kwa ujumla ni mdogo, ni manachama wachache wa kijiji watambua kila kitu kuhusu mikataba na makubaliano ya biashara ya utalii.

Arash

Katika kijiji cha Arash mapato yote yanabandikwa kwenye ubao wa matangazo. Hata hivyo asilimia 55 wanafahamu mapato ila wanasema serikali haiko wazi, asilimia 15 wanafahamu mapato kupitia mkutano mkuu na ubao wa matangazo na asilimia 15 hawajui lolote kuhusu mapato. Pia dhahiri kuna upungufu wa uelewa wa wajibu wa serikali ya kijiji miongoni mwa wanakijiji, na asilimia 15 ya uchunguzi wa kaya imeonyesha kuwa hawajui muundo wa utawala wala kamati ya maliasili, na asilimia 70 hawajui kitu chochote kuhusu muundo wa utawala wala wanachama wake, na ni asilimia 15 hawajui kuwa kamati maalumu inahusika katika utalii na maliasili.Arash wanaweka majina ya wanachama wote kwenye ubao wa matangazo wa ofisi ya kijiji pamoja na dhima na majukumu ya kamati.

Piyaya

Wakati wa uchunguzi wa kaya, asilimia 10 walifahamu kamati ya maliasili, na asilimia 90 imeonyesha kuwa hawafahamu sana muundo wa utawala kijijini, isipokuwa maarifa ya msingi waliyonayo kama vile mwenyekiti na katibu wa kijiji. Wahojiwa hawa hawaitambui kamati ya maliasili. Asilimia 55 ya kaya wamenena kuwa serikali haiko wazi kuhusu mapato. Asilimia 20 hawajui mapato ya utalii, na asilimia 25 imeonyesha wanajua mapato kupitia mkutano mkuu wa mwaka na ubao wa matangazo.

Engaresero

Katika kijiji cha Engaresero asilimia 25 ya kaya zilizopitiwa hawajui muundo wa utawala wowote mwingine, asilimia 45 wanajua kamati ya maliasili, asilimia 10 imeonyesha wanajua kamati maalumu ya utalii, huku asilimia 20 hawaamini kama kuna kamati kwa ajili ya usimamizi wa maliasili. Asilimia 60 nyingine ya kaya zilizopitiwa imeonyesha kuwa Serikali ya kijiji haiko wazi katika mapato, asilimia 5 wanajua hakuna mapato ya utalii na asilimia 35 imeonyesha kuwa wanajua mapato ya utalii kupitia mkutano mkuu wa mwaka. Waendesha utalii wawili waliopitiwa katika kijiji cha Engaresero hawafahamu mkataba uliopo kati ya kijiji na

kampuni ya uwindaji.

Pinyinyi

Katika kijiji cha Pinyinyi, uongozi wa kijiji umeiambia timu ya uchunguzi kuwa hakuna shughuli ya utalii inayofanyika katika kijiji chao. Hata hivyo, timu ya uchunguzi tena iliambiwa na kampuni ya wanyamapori Tanzania, mmoja wa waendeshaji utalii, mwenye mkataba na anayefanya shughuli ndogo za utalii katika kijiji cha Pinyinyi. Kati ya kaya zilizopitiwa,asilimia 90 wana uhakika kuwa hamna shughuli za utalii na hivyo hakuna mapato yaliyopatikana. Kwa kuongeza, asilimia 10 ya kaya wanadai hawajui kama kuna mapato yanayopatikana au la. Mbali na mapato,asilimia 55 ya kaya hawatambui muundo wa utawala wa kijiji.

Mapato ya utalii kwa vijiji

Mapato ya utalii wanayopata vijiji, pamoja na michango toka kwa waendeshaji utalii kwa ajili ya maendeleo ya kijiji na kuendeleza riziki ni muhimu sana kwa mafanikio ya utalii kwa vizazi vya baadaye. Uwajibikaji na uwazi wa muundo wa usimamizi unaohusika na mapato ni muhimu sana kusaidia jamii kushiriki kikamilifu na kusaidia sheria ndogondogo za kijiji na na kanuni nyingine zilizoundwa kulinda rasilimali za utalii, kama vile makazi ya wanyamapori.

Kama wanachama wa jamii hawaoni faida ya kiuchumi kutokana na utalii, hawawezi kuunga mkono kikamilifu mikataba ya biashara baina ya serikali ya kijiji na wawekezaji wa utalii. Wakati wa uchunguzi wa kaya, maoni yaliyokuwa yakijirudia rudia yaliibuka toka kwa wakazi mbalimbali katika vijiji vyote wanaomba uwazi zaidi katika mapato yanayokusanywa katika kila kijiji. Haya maombi kwa kiasi kikubwa ni matokeo ya uhaba wa habari waliyonayo wanakijiji kuhusu mikataba baina ya serikali ya kijiji na wafanya biashara ya utalii. Bila habari za kutosha wakazi wa kijiji wana msingi usio imara wa elimu kuhakiki uongozi wa kijiji na usimamizi wa mapato. Wachache wanajua zote asili na thamani ya uhisani ulioanzishwa kupitia biashara ya utalii iliyopo kijijini kwa maendeleo.

- Uchunguzi wa kaya **Arash** umeonyesha kuwa asilimia 10 ya wakazi wa kijiji walihudhuria mkutano wakati utalii na mikataba ikijadiliwa. Asilimia 20 ya wanachama walikuwa na mkataba zamani au walikutana na waendeshaji utalii, asilimia 25 wanafahamu michango kutokana biashara ya utalii, wakati asilimia 55 hawajui michango wowote na asilimia 20 inaonyesha kuwa hakuna michango.

- Katika **Piyaya**, uchunguzi wa kaya umeonyesha kuwa asilimia 30 hushiriki kwenye mkutano wakati utalii na mikataba inajadiliwa, na asilimia 60 ya wanachama wamekutana na waendeshaji utalii. Asilia 45 nyingine hawatambui michango kutoka biashara ya utalii na jinsi gani rasilimali zinatumiwa .

- **Engaresero** wana asilimia 30 hushiriki mkutano wowote unaojadili utalii lakini hakuna mikataba iliyojadiliwa, na asilimia 90 hawatambui michango kutoka biashara ya utalii. Kulingana na makubaliano na waendeshaji utalii, kijiji lazima kitoe risiti kwa mapato yanayolipwa kwa kijiji. Hata hivyo kwa zaidi ya miaka 3.5 iliyopita ya ubia, wafanya biashara ya utalii hawajapata risiti yeyote .

- Kijiji cha **Pinyinyi** wana shughuli chache za utalii. Ni mkataba mmja tu uliopo wa kampuni ya utalii wa uwindaji ambayo hutumia eneo mara chache. Hakuna kati ya wanachama waliosailiwa hawafahamu huu mkataba au michango yoyote au msaaada kutoka kwa kampuni .

5.5 MAENDELEO NA USIMAMIZI WA UTALII

Uchunguzi wa awali umepeleleza taratibu mbalimbali zilizopo zinazoruhusu serikali ya kijiji kusimamia mikataba na shughuli zenye kuhusu biashara ya utalii zinazofanyika katika vijiji.

Vijiji vyote isipokuwa Pinyinyi wana makubaliano ya mkataba zaidi ya mmoja na kampuni za utalii, baadhi ya hii mikataba imekuwepo ikifanya kazi zaidi ya miaka 10; mikataba mingine ni ya hivi karibuni. Piyaya wana Kampuni tatu (3), Arash wana mikataba miwili (2) na Engaresero wana mitatu (3).

Ufahamu wa makubaliano ya mikataba

Wawekezaji wote waliokaguliwa katika vijiji vya majaribio wana mikataba ya sasa. Kwa mujibu wa uongozi wa kijiji, mikataba hii inawasilisha masuala kwa upana kama vile kushiriki kwa jinsia, shughuli za kimila, athari za mazingira, kijamii na kiuchumi. Hata hivyo wafanyabiashara ya utalii wanatofautiana katika maoni, wananena kuwa kwa ukweli masuala haya hayapo katika mkataba (kutoa mkataba wa Arash).

Ufa huu unaonyesha kuwa kampuni za utalii na serikali ya kijiji hawana uelewa sawa wa wajibu na maudhui ya mikataba, kama inavyonekana zaidi kwa kujitokeza ukiukwaji wa ahadi za mikataba kwa pande zote mbili.

Ufahamu wa bidhaa/mazao ya utalii

Kila kijiji kina sehemu mbalimbali za vivutio vya utalii na shughuli za utalii zenye viwango tofauti. Hata hivyo, uchunguzi wa awali umeonyesha kuwa wanakijiji na viongozi hawana ufahamu wa tofauti kati ya makusudio na mazao mbalimbali, kwa hiyo itakua vigumu kwa pamoja kusimamia hali ya bidhaa hizi na kudalalia mikataba yoyote yenye utata katika njia ya kimkakati.

Muundo wa ada

Muundo wa ada unatofautiana kutoka kijiji hadi kijiji kwa bidhaa mbalimbali za utalii. Haikuweza kufahamika vizuri ni jinsi gani ada zilivyopatikana. Pia, ada zinazosimamiwa na mamlaka nyingine kama vile Idara ya wanyamapori na halmashauri za wilaya(kwa ada za viingilio langoni) zinatishia ushindani wa bidhaa za utalii.

Mawasiliano, dhima na majukumu

Uchunguzi wa awali umetambua upungufu wa fursa ya nafasi ya mawasiliano rasmi baina ya waendeshaji utalii na serikali ya kijiji. Waendeshaji utalii kijiji cha Piyaya wanafanya mkutano na uongozi wa kijiji mara tatu kwa mwaka, ingawa waendeshaji katika maeneo mengine wanapanga mkutano kwa kusudio maalumu. Hata hivyo, katika kijiji cha Piyaya na Arash wandeshaji utalii wameajiri afisa ushirikiano wa kijiji kurahisisha mawasiliano.

Pia, haiko wazi, dhima na wajibu wa waendeshaji utalii na serikali ya kijiji, kama inavyoonekana kwa upungufu wa ufahamu kuhusu mwongozo na kanuni kwa watekelezaji husika wa utalii. Ama mwongozo haupo au mwongozo uliopo ni tofauti kulingana na waendeshaji utalii na serikali ya kijiji. Pia ni dhahiri hakuna utaratibu wa kutathmini utendaji wa hizi sheria ndogondogo na mwongozo.

Utafiti umerekodi mfano mmoja tu wa usimamizi wa kijiji wa moja kwa moja wa bidhaa za utalii. Katika kijiji cha Engaresero serikali ya kijiji ilijaribu kukusanya ada kutoka kwa watalii kupitia waongozaji wageni wanaopanda mlima Lengai. Hata hivyo walishindwa kukusanya ada.

6. HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Utalii wenye dhamana unaweza kuwa chombo cha uchumi kwa uhifadhi wa maliasili. Kiambata muhimu kwa kuendeleza rasilimali za ardhi ya jamii ni uwezo wa mapato kuchangia ustawi wa jamii. Kwa njia hii jamii inayofaidika itathamini rasilimali hizi na kupata motisha ya kulinda na kuhifadhi kwa vizazi ya baadae. Mapitio ya awali yameonyesha kuwa kwa ujumla vijiji havina mpango wa matumizi ya ardhi, chombo ambacho kinasaidia kijiji kusimamia rasilimali na ugawaji wa ardhi kwa njia ya uwazi na ushirikishi. Itakuwa lazima kwa vijiji vyote kutengeneza mpango wa matumizi ya ardhi ili kuongoza viongozi waliopo na wanaofuata wanaohusika na usimamizi wa ardhi. Vema zaidi hii mipango ya matumizi ya ardhi ionyeshe ardhi itakayotumika kwa ajili ya shughuli za utalii.

Jinsi uongozi wa maliasili ndani ya kijiji unavyoshirikisha tawala tendaji zingine kama vile Idara ya wanyamapori, Mamlaka ya uhifadhi eneo la Ngorongoro na Hifadhi za Taifa Tanzania, inashauriwa kuimarisha mawasiliano baina ya wadau mbalimbali ili kujenga mshikamano wa mtazamo katika uhifadhi wa maliasili. Kuongeza sheria ndogondogo za kijiji lazima zisambazwe kwa wadau wote ili kutoa nafasi kwa pande zote kukubaliana. Uundaji zaidi wowote wa sheria ndogondogo, mwongozo na kanuni lazima zitengenezwe katika njia ya ushirikishi ili kupata majadiliano ya pamoja kutoka kwa wadau wote. Jitihada za uhifadhi wa pamoja zimefanikiwa katika kijiji kimoja na imetoa nafasi ya kuwezesha utambuzi na wajibu wa kulinda maliasili na kuimarisha wabia. Uchunguzi zaidi wa nafasi za uanzilishi wa kufanana lazima uzingatiwe.

Kwa kundi kubwa la wadau – wakazi wa vijiji vya Arash, Engaresero, Pinyinyi na Piyaya – uchunguzi wa awali umeonyesha mlolongo wa mapendekezo ya kuboresha ushirikishi na uwezo:

- Wanajamii wanahitaji mafunzo na msaada kuendeleza utawala bora na na usimamizi wa maliasili na maduhuli yatokanayo na utalii .
- Utafiti katika mifumo mbalimbali kwa viongozi wa kijiji kusambaza habari kwa jamii ipasavyo utatoa usalama wa mazingira kwa wajibu wa muda mrefu kwa jamii ambayo itatambua vema na hivyo kuhifadhi rasilimali hizi .
- Kuimarisha uwezo wa uongozi kujadili namna ya kuanzisha na kufunga mkataba kwa kutumia njia ya ushirikishi, kuendeleza uwezo wao ili kuimarisha na kuuza bidhaa zao itawasidia viongozi kujiamini wakati wa kufanya maamuzi, kuondoa wasiwasi wa biashara zao na mbia. La zaidi ,kuimarisha mawasiliano na wabia itaimarisha uhusiano wao, kutoa nafasi ya kushiriki na katika muda mrefu, kulinda hali ya uwekezaji .

Jamii inatakiwa kufahamu kuwa utalii ni biashara ambayo tayari wamewekeza.

Utalii wajibishi katika ardhi ya jamii ambayo unategemea maliasili zilizopo katika maeneo yao imekuwa ikiongezeka ikijulikana kwa neno jipya Utalii-stahili. Kuingia kwa mtazamo wa Utalii-stahili katika jamii na mazingira, wandeshaji utalii wamefikiria kutegemeana kwa uhifadhi wa maliasili, maendeleo ya maslahi ya jamii na biashara ya utalii.

Kwa mfano, ujasiriamali wa kati na mdogo waweza kuongeza unafuu wa bidhaa na huduma katika kambi za utalii zilizo kwenye maeneo yao; waendeshaji utalii wanaweza kuajiri zaidi wenyeji ndani ya kambi kusaidia faida itokanayo na utalii moja kwa moja iimarishe maslahi ya kaya: waendeshaji utalii, wakazi, na mamlaka za utawala wanaweza kuongeza uratibu na mawasiliano yao kuhifadhi maliasili. Chukulia upungufu ulipo wa kuanzisha utalii wa kijamii Tanzania kama ilivyoelezewa katika taarifa hii, utafiti zaidi juu ya nafasi ya wanajamii kufaidika kiuchumi katika njia ya adililifu na endelevu inahitajika.

Kwa Utalii endelevu katika vijiji vinne vilivyochunguzwa, miradi ya baadae na tafiti zitakazo tokana na huu utafiti wa awali unaweza kujumuishwa kusaidia kuongeza kushiriki kwa jamiii, maalumu kwa kupanga matumizi ya ardhi, kuchangia mawasiliano, kuchangia muundo wa usimamizi wa utalii, kuanzisha biashara ndogondogo, na kutengeneza kwa ujumla uwezo wa usimamizi kwa viongo wa eneo husika.

KUHUSU WASHIRIKI

Honeyguide Foundation ni shirika lisilo la kiserikali lisiloendeshwa kwa faida. Asasi hii ilianzishwa baada ya kujitokeza hitaji la asasi ambayo itakuwa kama kiungo kati ya wanajamii na sekta ya utalii ili pande zote mbili ziweze kupata faida kiuchumi. Na hivyo, amekuwa na mapenzi ya kiuhifadhi ya muda mrefu katika maeneo husika.

Ujamaa Community Resource Trust: Lengo lake ni kuimarisha upeo wa makabila machache Tanzania kaskazini, haswa wafugaji na wawindaji kama Maasai, Barabaig, Akie, Sonjo na Hadzabe, ila wanaweza kudhibiti, utawala na kufaidika kutokana na ardhi na rasilimali yao. Dhumuni moja la mkakati wao ni kukuza utalii ekologia katika jamii. Lengo kuu la UCRT ni kuboresha maisha ya jamii kwa njia ya kuboresha menejmenti ya ardhi na rasilimali. Mradi huu utaendelezwa na UCRT siku za badaye.

TasConsult ni kampuni ya ushauri katika maendeleo, hutoa ushauri katika mamlaka za mitaa, mashirika yasiyo ya kiserikali nchini na yale ya kimataifa. Inajihusisha na kujenga uwezo kwa ajili ya maendeleo, na huduma zake huhusisha kupanga mikakati, tathmini ya miradi na mchakato wa wadau wengi. Shirika pia huhusisha utaalamu katika kinga ya afya na huduma za kifedha na ina mtandao wa washauri watoao huduma za ziada.

Jumuiko la Maliasili Tanzania ni mtandao unaokua wa zaidi ya wanachama 1000, watu binafsi na mashirika huru ya kijamii ambayo yanafanya kazi katika sekta ya maliasili kwa kupitia kusaidia usimamizi wa maliasili endelevu na kipato cha kudumu. Kazi ya JMT kama wakala wa mabadiliko hufanywa kupitia vikundi tendaji vitatu katika maeneo yafuatayo: Misitu, Wanyamapori, Ufugaji, na Utalii wa kijamii.

© Damian Bell

© Jumuiko la Maliasili Tanzania 2009
SLP 15605 Arusha | Simu: +255 755 022267 | Nukushi: +1 815 550 2312 | B-pepe: info@tnrf.org | www.tnrf.org